twani mwake.
21 Msishindwe na uovu, illa mshinde uovu
**kwa** wema.
XIII. Killa mtu azitii nguvu zilizo juu, kwa-
ni nguvu hapana, isipokuwa kwa Muungu,
2 nguvu zilizo zimeamriwa na Muungu. Nao
wanaoziasi nguvu waiasi amri ya Muungu,
3 nao waasio wajiletea hukumu. Watawalao
si kuogofya katika tendo jema, illa katika
baya. Ukipenda usiogope nguvu, tenda ve-
4 ma, utakuwa na kusifiwa naye. Kwani ni
mtumishi wake Muungu kwako kwa mema.
Ukitenda vibaya, ogope, kwani hachukui u-
panga burre, ni mtumishi wake Muungu a-
5 mlipiaye hasira atendaye vibaya. Hivi shar-
ti mtii, si kwa hasira tu, illa kwa moyo.
6 Kwa hiyo tena mwatoa kodi, kwani hawa
wenyi amri kwa Muungu wakingoja hiyo-
hiyo.
7 Mlipe killa mtu alivyopaswa, yule wa ko-
8 di, kodi, yule wa ushuru, ushuru, yule wa
kuogofya kuogopa, yule wa heshima heshi-
9 ma. Msiwiwe na mtu cho chote, illa ku-
pendana, kwani ampendaye mtu, ameitimiza



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

sheria. Kwani ile, Usizini, usiue, usiibe,
usitamani, na amri ngineyo yote, katika ne-
no hili imejumlishwa, katika hili, Umpende
10 jirani wako kama moyo wako. Ampendaye
jirani hamtendei vibaya, bassi kupenda ni
timizo la sheria.
11 Na haya mkiujua wakati, kama sasa saa
sisi tuamke katika usingizi, kwani wokovu
12 wetu leo karibu, kuliko tulipoamini. Usiku
unapita, mchana karibu, tuvue matendo ya
13 giza, tuvae selaha za weupe. Kama mcha-
na tutembee kwa taratibu, si katika kula na
kulewa, si katika asharati na jeuri, si kati-
14 ka ugomvi na uwivu, illa vaeni Bwana Isa
Masiya, wala msifanye fikara za mwili kwa
tamaa.
XIV. Aliye thaifu mkaribisheni katika imani, si
kuyapambanua maswali.
2 Huyu athubutu kula vyote, huyu aliye
3 thaifu hula mboga. Alaye asimtharau asi-
yekula, wala asiyekula asimhukumu alaye,
kwani Muungu amkubaliye.
4 Nani wewe umhukumuye mtumwa wa
mwenyewe; kwa bwana wake yeye husima-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

ma ao kuanguka. Atasimamishwa, kwani
Muungu awezaye kumsimamisha.
5 Huyu achagua katika siku na siku, huyu
achagua killa siku. Killa mtu athubutike
6 katika nia yake. Aifikiriye siku, kwa Bwa-
na hufikiri, asiyeifikiri siku, kwa Bwana ha-
fikiri. Alaye, hula kwa Bwana, akimshu-
kuru Muungu, asiyekula, kwa Bwana hali,
7 naye amshukuru Muungu. Hakuna kwetu
aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye
8 kwa nafsi yake. Tukiishi, kwa Bwana twai-
shi, tukifa, kwa Bwana twafa. Bassi tu-
9 kiishi, tukifa, aliye naswi Bwana. Kwa hiyo
Masiya alikufa akafufuka, awamiliki na wa-
fu na wahayi.
10 Mbona wewe wamhukumu ndugu yako?
ama wewe wamtharau ndugu wako? kwani
11 wote tutasimama kitini pa Muungu. Kwani
imeandikwa, Mimi hayi, anena Bwana, ya
kwamba litanikunjia killa gote, na killa uli-
12 mi utamwungamia Muungu. Bassi tena
sisi killa mmoja wetu atatoa hesabu yake
kwa Muungu.
13 Bassi tusihukumiane, illa afathali tuhu-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

kumu ndugu asitiwe ukwazo wala chu-
kizo.
14 Najua, nikimtumainia Bwana Isa, kama
hakuna kitu chenyi unajisi chenyewe, illa
kwake akionyaye cha unajisi, kinao unajisi.
15 Ndugu wako akihuzunika kwa chakula
chako, huendi katika kupendana. Usimha-
ribu kwa chakula chako Masiya aliyekufa
kwa ajili yake.
16 Jema lenu lisinenwe unajisi, (17) kwani
ufalme wa Muungu si chakula na kunywa,
illa haki, na amani, na furaha katika Roho
18 Mtakatifu, kwani amtumikiaye Masiya hi-
vi, hupendeza Muungu husifiwa tena na
watu.
19 Bassi fuateni mambo ya amani, nayo ya
20 kujengeana. Kwa ajili ya chakula usihari-
bu kazi yake Muungu.
Yote safi, illa mabaya kwake alaye kwa
21 kujikwaa. Ni heri kutoa kula nyama, na
kunywa mvinyo, ama *yote* yamkwazayo
ndugu, ao yamchukizishayo, ao yamthoofi-
shayo.
22 Unayo imani? Uwe nayo mwenyewe



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is
machoni pa Muungu. Amebarikiwa asiye-
23 jihukumu katika alikubalilo. Apambanuaye
huhukumiwa akila, kwani silo la imani, lisi-
lo la imani lote ni thambi.

XV. Imetupasa sisi tulio hodari kuchukua u-
thaifu wao wasio na nguvu, wala si kujipe-
2 ndeza, killa wetu ampendeze jirani wake
3 kwa kujengea. Kwani Masiya hakujipe-
ndeza mwenyewe, illa kama ilvyoandikwa,
Mashutumu yao waliokushutumu yamenia-
ngukia mimi.

4 Yalioandikwa zamani yameandikwa kwa
mafundisho yetu, tupate kwa uvumilivu na
faraja ya maandiko kuwa na tumaini.

5 Muungu wa uvumilivu na faraja awa-
jalie kuwaza mamoja ninyi kwa ninyi kati-
6 ka Masiya Isa, mpate wenyi moyo mmoja
kwa kinwa kimoja kumtukuza Muungu na
7 Baba wa Bwana wetu Isa Masiya. Kwa
hiyo mkubaliane, kama Masiya alivyotuku-
bali kwa utukufu wake Muungu.

8 Kwani nasema Isa Masiya amekuwa
mngoje wa tohara kwa ajili ya kweli yake
9 Muungu, afanye imara ahadi zao baba, illi


Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

mataifa wamtukuze Muungu kwa ajili ya
rehema, kama ilivyoandikwa, Kwa hiyo
nitakuungama katika mataifa na kwa jina
10 lako nitaimba. Na tena anena, Mpendeze-
11 we, mataifa, pamoja na watu wake. Na tena,
Msifuni Bwana, mataifa yote, mtukuzeni,
12 enyi watu wote. Na tena Isaya anena, Li-
takuwa shina la Yesse, naye atakayesimama
kuwatawala mataifa, ndiye mataifa wataka-
yemtumainia.

13 Muungu wa tumaini awajaze na furaha yo-
te na amani, katika kuamini, mzidi ninyi
katika tumaini na nguvu za Roho Mtakati-
fu.

14 Nimethubutika mimi, ndugu zangu, juu
yenu, kama ninyi mmejaa wema, mkijali-
zwa na elimu yote, mkiweza na kujifundi-
15 shana. Nimewaandikia ndugu pasipo hofu,
kwa sehemu, kama kuwakumbusha, kwa
neema niliyopewa na Muungu, niwe mimi
16 wakili wa Masiya Isa, kwa mataifa, nikifa-
nya kazi ya mkohani wa anjili ya Muungu,
sadaka za mataifa zikubalike, zikitakaswa
katika Roho Mtakatifu.



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is